**HOTUBA YA MHE. JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA SHEREHE YA 69 YA KUWAKUBALI NA KUWAPOKEA MAWAKILI WAPYA 279 KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA MWALIMU NYERERE, DAR ES SALAAM, TAREHE 01 DESEMBA, 2023**

---

- **Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;**
- **Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania;**
- **Mhe.Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi, Mahakama Kuu ya Tanzania;**
- **Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania;**
- **Prof. Sist Joseph Mramba, Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo;**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Sheria;**
- **Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama;**
- **Mheshimiwa Sylvester Joseph Kainda, Msajili Mahakama ya Rufani;**
- **Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka;**
- **Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali;**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

- **Wakili Harold Giliard Sungusia, Rais wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea (TLS);**
- **Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa;**
- **Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Sasa na Wastaafu mliopo;**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini mliopo;**
- **Waheshimiwa Wasajili, Manaibu Wasajili, Watendaji na Mahakimu;**
- **Wakili Edward Charles Heche, Mwenyekiti wa Umoja wa Mawakili Vijana TLS;**
- **Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea;**
- **Ndugu Wanahabari;**
- **Wageni Waalikwa; na**
- **Mabibi na Mabwana.**

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sote kuwepo hapa leo katika sherehe hii ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili Wapya 279 tukiwa na afya njema. Nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa heshima uliyonipatia ya kunialika na kunipatia nafasi ya kutoa salamu za pongezi kwa Mawakili hawa siku ya leo.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Naipongeza sana Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na wadau wote waliofanikisha na kuwawezesha hawa Mawakili Wapya kufikia hatua ya kukubaliwa na kupokelewa kuwa Mawakili siku ya leo hivyo, kufanikisha ndoto zao. Mawakili Wapya hongereni sana kwa kukubaliwa na kupokelewa leo kuwa Mawakili wa Kujitegemea, **KARIBUNI KATIKA TAALUMA HII ILIYOTUKA.**

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Tumekusanyika hapa kwa lengo la kuwapokea na kuwakubali Mawakili Wapya wapatao 279. Pamoja na pongezi, naomba nitumie nafasi hii kuwashirikisha Mawakili hawa wapya mambo machache wanayopaswa kuzingatia watakapokuwa

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

wakitekeleza majukumu ya Uwakili wa Kujitegemea baada ya kusajiliwa katika Daftari la Mawakili.

Niwakumbushe mawakili wenzangu kuwa, mkiwa Mawakili, mnapaswa kutambua kuwa jukumu la utoaji haki ni sehemu muhimu ya maendeleo ya nchi na watu wake katika kuimarisha Utawala wa Sheria na misingi ya utawala bora. Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inabainisha kuwa Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa Mahakama. Nafurahi kuona Mawakili 279 leo mnaungana nasi katika kipindi hiki ambacho Serikali yetu tukuka imeshawezesha na inaendelea kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama ambapo leo kuna Vituo Jumuishi katika mikoa mbalimbali nchini vya kutolea Haki kwa wadau kwa mujibu wa sheria na kwa wakati.

Kumbukeni kuwa, Mawakili ni Maafisa wa Mahakama kwa mujibu wa kifungu cha 66 cha Sheria ya Mawakili, Sura ya 341. Kwa nafasi hiyo, tumepewa dhamana ya kuisaidia Mahakama kufikia maamuzi ya haki na kwa wakati. Aidha, kanuni ya 92 ya Kanuni za Maadili na Mienendo ya Mawakili, Tangazo la Serikali Na. 118 la

YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

mwaka 2018 inakataza hujuma dhidi ya Mahakama katika utoaji haki. Vitendo vya hujuma ni pamoja na utoaji wa taarifa za uongo au kufanya jambo litakaloipotosha Mahakama au Baraza kufikia maamuzi ambayo yasingefikiwa endapo upotoshaji huo usingekuwepo. Aidha, kanuni ya 137 ya Kanuni hizo inatukataza mawakili kutoa maoni katika kesi iliyo mahakamani katika namna inayoweza kuathiri matokeo ya kesi husika.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Naomba niwasihi Mawakili kuzingatia kukumbuka kuwa, Tasnia ya Sheria ni nyeti na muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Mawakili mliokubaliwa na kupokelewa leo mnapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali mnapotekeleza majukumu yenu, hususan, Kanuni zote za Maadili na Mienendo ya Mawakili katika Tangazo la Serikali Na. 118 za mwaka 2018. Mkumbuke kuwa, Kiapo cha Uadilifu mlichoapa leo ndio dira yenu na daima kiwakumbushe umuhimu wa kuheshimu maadili ya kazi yenu ya Uwakili mtakayopaswa kuifanya kwa weledi na uaminifu.

Nawakumbusha kuwa, kumekuwa na tuhuma kwa baadhi ya Mawakili wa Kujitegemea kujihusisha na vitendo vya rushwa na udanganyifu kwa maslahi yao

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU

binafsi, ikiwemo kuwasaliti wateja wao kwa kupokea rushwa, kutohudhuria mahakamani, kutotunza siri za wateja, kutokuwepo kwa mawasiliano mazuri baina ya wakili na mteja, kutotumia vizuri fedha za wateja kwa ajili ya kazi iliyokusudiwa na kutumia mihuri isivyo halali katika kufanya kazi za uwakili. Vitendo vya ukiukaji maadili ya kazi ya uwakili pamoja na vitendo vya watu wasio na sifa ya kufanya kazi ya uwakili bila kuwa na sifa za uwakili, havivumiliki na haviwezi kufumbiwa macho.

Mtakumbuka kuwa, mnamo tarehe 31 Oktoba, 2023 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Mbili pamoja na mambo mengine, lilipitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria (Na. 11) ya 2023 (the Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Act. No. 11 of 2023) ambayo ilirekebisha kifungu cha 42 cha Sheria ya Mawakili, Sura 341 kwa lengo la kupambana na mawakili vishoka. Marekebisho hayo yameweka adhabu kwa mtu atakayefanya kazi ya uwakili bila kuwa na sifa za uwakili kuwa ni kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu jela au vyote kwa pamoja, yaani faini na kifungo. Hatua hii ni tofauti

na awali ambapo adhabu ilikuwa ni kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja jela au vyote kwa pamoja. Katika muktadha huo nitumie fursa hii kuwaonya wale ambao wamekuwa wakifanya hivyo kuacha mara moja tabia hiyo na nyinyi muungane nasi kutokomeza vitendo hivyo vya ukengeufu wa maadili.

Aidha, ili kulinda heshima ya taaluma ya sheria, natoa wito kwa Kamati ya Maadili ya Mawakili kuendelea kuchukua hatua za kinidhamu na kwa mujibu wa utaratibu ulioanishwa katika kifungu cha 13 cha Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 na Kanuni zote za Maadili na Mienendo ya Mawakili katika Tangazo la Serikali Na. 118 za mwaka 2018 dhidi ya Mawakili wa Kujitegemea wanaoharibu heshima ya taaluma ya sheria kwa kukosa uadilifu na maadili, na dhidi ya mawakili vishoka.

Naomba kunukuu maneno ya Lord Reid aliyoyatoa katika kesi ya **Rondel vs. Worsley** [1969] 1 A.C 191 katika uk. 227; [1967] All E.R 993 katika uk. 998 kuhusu wajibu wa Wakili kwa mteja na Mahakama, nikiwashauri Mawakili walioapishwa leo kuzingatia maneno hayo:

> **"Every Counsel has a duty to his client fearlessly to raise every issue, advance every argument and ask every question, however**



HOTUBA YA MW...

**distasteful, which he thinks will help his client's case. But, as an officer of the Court concerned in the administration of justice, he has an overriding duty to the Court, to the standards of his profession, and to the public, which may and often does lead to a conflict with his client's wishes or with what the client thinks are his personal interests. Counsel must not mislead the court, he must not lend himself to casting aspersions on the other party or witnesses for which there is no sufficient basis in the information in his possession, he must not withhold authorities or documents which may tell against his clients but which the law or the standards of his profession require him to produce".**

Tafsiri isiyo rasmi ya nukuu hiyo kwa lugha ya Kiswahili ni kwamba:

**"Kila wakili, bila woga, ana wajibu kwa mteja wake kuuliza swali lolote, kuibua hoja yoyote hata kama ni ya kuchukiza, ambayo anadhani itasaidia shauri la mteja wake. Lakini, kama Afisa wa Mahakama anayehusika katika utoaji haki, anao wajibu mkuu wa kwanza kwa Mahakama, kwa viwango vya taaluma yake, na kwa**

HOT MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**umma, ambavyo vyaweza na mara nyingi kusababisha mgongano dhidi ya matakwa ya mteja wake au kile mteja anadhani ni kwa maslahi yake binafsi. Wakili hapaswi kuipotosha mahakama, asijiingize katika kufifisha matamanio ya upande pinzani au mashahidi wake pasipokuwa na sababu ya msingi kulingana na taarifa alizonazo, hapaswi kuficha sheria/tafsiri au nyaraka ambazo zaweza kuwa kinyume na maslahi ya mteja wake, bali, kadri sheria au viwango vya taaluma yake vinavyomtaka kuziwasilisha".**

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Wizara ya Katiba na Sheria, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Serikali na Taasisi binafsi, inatekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (*Mama Samia Legal Aid Campaign*) ambayo ilizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), tarehe 27 Aprili, 2023. Kampeni hiyo ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu ilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wasiomudu gharama za Mawakili wa Kujitegemea. Kwa kuwa Kampeni hii inatekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini, natoa rai kwa Mawakili

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

waliokubaliwa na kupokelewa leo kuungana na Mawakili waliowatangulia kuwasaidia wananchi wasiomudu gharama za kuwalipa Mawakili ili kusaidia utekelezaji wa Kampeni hiyo huku wakipata fursa ya kutumia elimu yao ya kutatua migogoro ya kisheria na hivyo kuwawezesha wahitaji wa haki, hususan, watoto, wanawake na makundi maalum kupata haki kwa wakati.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Utakumbuka kuwa, tarehe 29 Septemba, 2022, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akizindua Chama cha Mawakili wa Serikali, pamoja na mambo mengine, aliwataka Mawakili wa Serikali kuhakikisha migogoro inatatuliwa kabla ya kufikishwa mahakamani. Kufuatia maelekezo hayo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na taasisi nyingine za umma na binafsi wanaendelea kutekeleza maelekezo hayo ili kupunguza gharama, mrundikano wa mashauri na muda wa kutatua migogoro mbalimbali ndani na nje ya nchi. Nawashauri Mawakili Wapya mliokubaliwa na kupokelewa leo muwafahamishe wateja wenu kuhusu uwepo wa nafasi ya kutatua migogoro yao nje ya Mahakama kulingana na

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

mazingira ya mashauri husika na kwa kuzingatia matakwa yaliyobainishwa katika Katiba, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na matakwa ya kanuni za 58 na 59 za Kanuni za Maadili za Mawakili, Tangazo la Serikali Na. 118 za mwaka 2018. Siyo jambo lenye tija kwa mteja wake inapotokea wakili kupuuza Kanuni tajwa na kung'ang'ania kuendesha mahakamani shauri ambalo linaweza kuhitimishwa kwa usuluhishi.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Kwa kuwa taaluma ya sheria inahitaji Mawakili wenye ujuzi na uzoefu ili kuhakikisha haki za wananchi zinalindwa, ni vema tufahamu kuwa ni jukumu letu sisi Mawakili Waandamizi kuwajengea uwezo (mentorship) Mawakili Wapya kwa kuwapatia miongozo, maelekezo na ushauri stahiki ili waweze kufahamu mila, desturi, taratibu na maadili ya kuzingatiwa na maafisa wa mahakama na wanachama wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea.

Nitumie tena fursa hii kunukuu maneno ya nasaha kutoka katika katika Makala iliyoandikwa na William J. Teggart kuhusu ushauri wake kwa mawakili vijana nchini Marekani aliponukuu maneno kutoka kitabu cha Allen Dershowitz kiitwacho 'Letters to a Young Lawyer' (2005), kutoka aya ya kwanza yasemanyo:



HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**"We graduate from law school knowing the law from an academic perspective but not from a practical perspective. We learn how to practice law by learning from others and actually doing it. A mentor can impart good habits and teach us skills that we will use in our entire career".**

Tafsiri isiyo rasmi ya nukuu hiyo kwa lugha ya Kiswahili ni kwamba:

**"Tunahitimu katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo tukiwa tumeijua sheria kwa mtazamo wa kitaaluma na si katika mtazamo wa kivitendo. Tunajifunza jinsi ya kutumia sheria kwa kujifunza kutoka kwa wengine na kwa hakika kwa kufanya kwa vitendo. Mshauri MBOBEVU anaweza kuturithisha tabia njema na kutupatia maarifa tutakayotumia katika kipindi chote tutakachotekeleza majukumu yetu kazini".**

Mawakili pya mnapaswa kufahamu kuwa, hamjakubaliwa na kupokelewa kuwa Mawakili wa Kujitegemea kwa sababu tu mlifaulu mitihani yenu, bali, kwa kuwa mmeonekana kuwa na uwezo na tabia njema. Katika Hotuba aliyoitoa mnamo

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

tarehe 21 Agosti, 2023, Rais wa Chama cha Sheria Singapore JASON CHAN TAI-HUI SC alisema maneno yafuatayo, ninanukuu kutoka ukurasa wa pili:

> **"You are not called to the Bar to act as a chatbot. It is now your responsibility to listen closely to the question and, before giving your views, assess why the question was asked in the first place. In other words, you must do more than quote the contents of a statute, a case or a textbook when answering questions. Instead, apply your training and experience to find solutions to the problem at hand. Provide advice that will help to further or achieve the goal that lies at the heart of the question. Rather than legal knowledge alone, it is innovative solutions that will be the hallmark of legal practice for your generation of lawyers. I hope that you will embrace a mindset of creativity, curiosity and constant learning from the very beginning of your careers".**

Tafsiri isiyo rasmi ya lugha ya Kiswahili ya nukuu hiyo ni kwamba:

> **"Hamjakubaliwa na kupokelewa kuwa Mawakili ili kufanya kazi kama zilivyo programu za akili bandia. Ni jukumu lenu sasa kusikiliza swali kwa makini na kabla ya kutoa maoni yenu,**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**kutathmini kwa nini swali hilo liliulizwa. Kwa maneno mengine, ni lazima mfanye zaidi ya kunukuu yaliyomo katika sheria, kesi au kitabu cha ziada/kiada unapojibu maswali. Badala yake, tumieni mafunzo na uzoefu wenu katika kutafuta suluhisho la tatizo husika. Toa ushauri utakaoelekea au utakaotatua kiini cha tatizo. Mbali na maarifa ya kisheria pekee, ni ubunifu katika kutafuta majibu ya matatizo ambayo yatakuwa msingi/alama mahsusi ya utendaji wa kazi za kisheria katika kizazi chenu cha wanasheria. Natumaini kuwa mtafungamana na mawazo ya akili ya ubunifu, udadisi na kujifunza kusiko na kikomo mara tu mnapoanza utekelezaji wa majukumu ya kazi zenu."**

Naendelea kusisitiza kwamba, Mafunzo elekezi kutoka kwa Mawakili Waandamizi ni muhimu sana kwa sababu yatawasaidia Mawakili Wapya kupata uelewa, maarifa na stadi mbalimbali za namna ya kutekeleza majukumu yao kwa haraka na kwa ufanisi. Aidha, Baraza la Uongozi la TLS linapaswa kuweka utaratibu maalum kwa kuwataka Mawakili Waandamizi kuweka mipango na mikakati ya kuwajengea

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

uwezo Mawakili Wapya ili kuwapatia stadi na uelewa mpana wa sheria na hivyo kulinda hadhi asili ya Tasnia ya Sheria.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Kwa kuzingatia kuwa jukumu la kukiimarisha Chama cha Mawakili Tanganyika na kujenga uwezo wa mawakili wake ni endelevu hasa kipindi hiki ambacho mawakili wetu wanatakiwa kupanua wigo wa kutoa huduma na kufungua ofisi au matawi nje ya nchi, hivi karibuni Serikali ilifanyia kazi maombi ya siku nyingi ya kuiwezesha TLS kuwa na Uongozi unaokaa madarakani kwa kipindi kinachowezesha kusimamia Mpango Mkakati wa Chama na mipango mingine tofauti na mwaka mmoja mmoja ambao umetumika kwa miaka mingi. Kwa msingi huo, kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria (Na. 11) ya 2023 (the Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Act. (No. 11) of 2023) iliifanyia marekebisho Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura 307 (The Tanganyika Law Society Act, Cap.307) kupitia kifungu cha 15(3) na (5) ili kuongeza sifa za wajumbe wa Baraza la Uongozi la TLS pamoja na kuongeza muda wa wajumbe wa Baraza la Uongozi wa TLS kuwa madarakani kutoka mwaka mmoja kuwa miaka mitatu. Kama nilivyoeleza, lengo la marekebisho hayo

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

ni kuimarisha Uongozi na kuweka muda wa kutosha kwa viongozi kutekeleza vipaumbele vya Baraza.

Ni matarajio yangu kwamba, Baraza la Uongozi la TLS na Mawakili wote waandamizi sasa mtaweka Mpango na Mkakati wa namna ya kuwalea mawakili vijana, wakiwemo Mawakili 279 walio mbele yetu leo. Aidha, kwa kuwa Serikali inatambua mchango wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) katika kuimarisha na kudumisha Utawala wa Sheria nchini, niruhusu nitoe wito kwa Uongozi na Wanachama wa TLS kuweka kipaumbele na kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali kwa kushiriki katika programu mbalimbali zinazoratibiwa na Serikali. Ni dhahiri kuwa mchango wa Wanachama wa TLS ni muhimu katika kuimarisha Utawala wa Sheria na misingi ya utawala bora nchini.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Ninapoelekea kuhitimisha salamu zangu, naomba uniruhusu pia kutoa rai kwa Mawakili wa Serikali na wa Kujitegemea kushirikiana kwa karibu na wadau weingine kuhakikisha kwamba wanazingatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Haki Jinai katika kuangalia jinsi ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini ambayo ilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 31 Januari, 2023 chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu Mstaafu ambayo ilikabidhi Taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais tarehe 15 Julai, 2023. Kutokana na mabadiliko makubwa na ya haraka ya kiuchumi, kiteknolojia, kisiasa, kijamii na hata kiutamaduni ambayo yanahitaji kwenda sambamba na mabadiliko ya sheria, nawaasa maafisa wa mahakama na Mawakili wote kujiendeleza kimasomo, hususan, katika fani mtambuka. Aidha, ni jambo la kupigiwa chapuo kwamba Wakili anapaswa kujituma, kufanya tafiti, kuongeza uadilifu na kuwajibika kwa kuzingatia kwamba Mawakili ni Maafisa wa Haki, na hivyo kipaumbele chao kinapaswa kuwa ni utoaji na usimamiaji wa haki na siyo fedha. Mawakili wa Serikali na wa Kujitegemea wanapaswa kushirikiana kwa maslahi ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.

Mnamo tarehe 8 Novemba, 2023 nilifarijika kupokea mrejesho kutoka kwa afisa mmoja wa Mahakama aliyebahatika kupata mafunzo katika kada tofauti na utoaji wa maamuzi ambayo pamoja na mambo mengine, yalihusisha namna ya kujenga uwezo katika upelelezi wa makosa ya jinai. Katika ujumbe wake afisa huyo alinipatia mrejesho ufuatao:

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**“…niliweza kujifunza kuhusu uchunguzi. …Lakini nimegundua pia baadhi ya wanasheria hawatekelezi majukumu yao ipasavyo….Sasa hivi naelewa maana ya usemi kwamba Ushahidi haujakamilika kwa sababu nimejua jinsi ilivyo vigumu kukusanya Ushahidi.”**

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Hafla hii ya kuwaapisha na kuwakubali Mawakili Wapya inakwenda sambamba na maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe Mosi Desemba, Hivyo, ni vema tuendelee kukumbushana kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam wetu kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa huu unaohatarisha maisha ya watu ulimwenguni kote na hivyo kufifisha nguvukazi ya Taifa.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Baada ya kusema hayo, nawapongeza tena Mawakili Wapya wa Kujitegemea mliokubaliwa na kupokelewa siku ya leo na hatimaye mtakuwa Mawakili wa Kujitegemea, Maafisa wa Mahakama na Wanachama wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) baada ya kukamilisha taratibu za kisheria. Kwa upande wetu, Serikali yenye Wanachama 3,353 kwenye Chama ya Mawakili wa Serikali (1,663

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

wakiwa pia Wanachama wa TLS), tunaahidi kufanya kazi na kuwapatia ushirikiano wote Mawakili 279 mliokubaliwa leo na wale watakaopenda baada ya kutimiza vigezo vya ajira kujiunga nasi katika Utumishi wa Umma.

Sasa nimalizie kwa kuwatakia wote Sikukuu Njema za mwisho wa mwaka, 2023 na Kheri ya Mwaka Mpya wa 2024.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
1 Desemba, 2023

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI